# GEITA GOLD MINING LIMITED (GGML) KILIMANJARO CHALLENGE DHIDI YA VVU NA UKIMWI

## "Kili Challenge"

TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA COMMISSION FOR AIDS TACAIDS

Kilimanjaro HIV&AIDS Challenge
Tuko Pamoja • We Are Together

ANGLOGOLDASHANTI
GEITA GOLD MINE TANZANIA

**Kumb. Na. AE.179/222/01/29**

# TANGAZO LA MAOMBI YA RUZUKU ZA UFADHILI CHINI YA MFUKO WA KILI CHALLENGE WA GGML KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA AFUA ZA VVU NA UKIMWI TANZANIA BARA

**Tarehe: 24 Machi, 2025**

**1. Utangulizi**

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), kupitia ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi (PPP), inaratibu programu ya Kili Challenge dhidi ya VVU na UKIMWI. Programu hii hufanyika kila mwaka kwa lengo la kukusanya fedha ili kufadhili wapanda mlima Kilimanjaro na kusaidia utekelezaji wa shughuli za VVU na UKIMWI. Fedha zinazopatikana kupitia programu ya Kili Challenge hutolewa kama ruzuku kwa mashirika, jamii zilizo hatarini kupata maambukizi ya VVU na watu binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za VVU na UKIMWI.

Programu ya Kili Challenge ilianzishwa na kampuni ya GGML mwaka 2001 na imekuwa ikiendelea hadi sasa, utekelezaji wake unazingatia sera za VVU na UKIMWI, mikakati ya kitaifa, na miongozo mingine inayohusiana na VVU na UKIMWI ili kuendana na vipaumbele vya kitaifa vya afya na VVU/UKIMWI.

TACAIDS ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 22 ya mwaka 2001, ambapo Kifungu cha 5(1.d) kimeipa mamlaka ya kutoa uongozi wa kimkakati katika mwitikio wa VVU na UKIMWI, kushirikiana na wadau katika kutafuta na kugawa rasilimali kwa ajili ya VVU na UKIMWI, pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini juu ya mwitikio wa kitaifa wa kisekta dhidi ya UKIMWI Tanzania Bara.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Kili Challenge imetenga jumla ya **Tshs. 600,000,000** (Shilingi Milioni Mia Sita) kwa ajili ya ruzuku za kusaidia juhudi katika mwitikio wa VVU na UKIMWI. Fedha hizi zitatumika kusaidia utekelezaji wa afua mbalimbali, hususan kwa wachimba madini wadogo wadogo katika mkoa wa Geita, vikundi vya Watu Wanaoishi na VVU (PLHIV), vituo vya kulelea yatima, Mfuko wa UKIMWI (ATF), Vituo vya maarifa vilivyo kando kando ya Barabara kuu (Roadside Wellness Centers), na programu za kuhamasisha vijana kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU.

Hata hivyo, kwa tangazo hili jumla ya shilingi **Tshs. 150,000,000 (Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini)** zimetengwa mahsusi kwa ajili ya kusaidia vikundi vya Watu wanaoishi na VVU (WAVIU) katika utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI.

Walengwa wakuu wa Ruzuku ya Kili Challenge ni:

- Watu Wanaoishi na VVU (WAVIU)
- Wajane na Wagane
- Watoto Yatima na Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (MVC & OVC)
- Wachimbaji wadogo wadogo wa madini
- Wavuvi
- Wafanyakazi wa mashambani
- Madereva wa masafa marefu na jamii zinazoishi kandokando ya barabara kuu
- Wasichana Balehe na Wanawake Vijana (AGYW)
- Wavulana Balehe na Wanaume Vijana (ABYM)

Mashirika yanayotoa huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi haya yanastahili kupokea ufadhili kwa ajili ya kutekeleza afua za kinga, matunzo na tiba ya VVU, elimu kuhusu VVU na UKIMWI, pamoja na ulinzi wa kijamii, ikiwa ni pamoja na shughuli za WAVIU za kujiongezea kipato.

Ruzuku hii inasimamiwa na Bodi ya Wadhamini wa Kili Challenge na inasambazwa kwa walengwa kupitia TACAIDS. Waombaji wanaostahili ni mashirika yaliyosajiliwa na yanayofanya kazi ndani ya Tanzania Bara.

**2. Hatua Zinazofadhiliwa Chini ya Ruzuku ya Programu ya Kili Challenge**

Ruzuku za programu ya Kili Challenge zinalenga kusaidia utekelezaji wa shughuli zenye matokeo makubwa zinazochangia juhudi za muda mrefu kulingana na Mkakati wa Tano wa Kitaifa wa VVU na UKIMWI wa mwaka 2021–2026. Mkakati huo unalenga kufanikisha malengo makuu ya kitaifa, ikiwemo:

- Kupunguza maambukizi mapya ya VVU hadi kufikia chini ya 15,000 ifikapo 2026
- Kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI hadi kufikia 17,913 ifikapo 2026
- Kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto hadi kufikia chini ya asilimia 4 ifikapo 2026
- Kutokomeza unyanyapaa unaohusiana na VVU na UKIMWI ifikapo 2026

Haya ni matokeo muhimu ambayo Tanzania imejidhatiti kuyafanikisha katika muda mfupi ujao. Kupitia ufadhili huu, kipaumbele kitatolewa kwa maeneo yafuatayo:

- Kutoa msaada wa moja kwa moja kwa jamii zilizoathirika na zinazokabiliwa na maambukizi ya VVU ili kutokomeza UKIMWI
- Kupunguza athari za VVU na UKIMWI kwa makundi yaliyo hatarini
- Kuongeza upatikanaji wa fursa za uwezeshaji kiuchumi kupitia shughuli za uzalishaji kipato (IGAs)
- Kuongeza na kuboresha huduma za kinga dhidi ya VVU, hasa kwa makundi yaliyo hatarini
- Kuboresha upatikanaji wa matibabu ya VVU, huduma za uangalizi na kuhakikisha wagonjwa wanadumu katika matibabu, hasa kwa makundi yaliyo hatarini
- Kukuza na kuboresha haki na ulinzi wa watu wanaoishi na VVU (WAVIU) na makundi mengine yaliyo hatarini
- Kuboresha uwezo wa serikali katika kufadhili mipango ya ndani ya VVU na UKIMWI kwa njia endelevu
- Kuongeza uelewa wa kina wa VVU miongoni mwa makundi yote ya jamii
- Kuhamasisha na kupanua mbinu bora za kukabiliana na VVU kwa kuhakikisha ushirikiano wa wadau wote, wakiwemo WAVIU, taasisi binafsi na za umma
- Kuweka mifano ya utekelezaji inayoweza kurudiwa na kupanuliwa kwa ajili ya kujifunza na kuboresha mbinu za kukuza mwitikio wa VVU na UKIMWI

**3. Kanuni Zinazoongoza Utoaji wa Ruzuku**

- Muda wa ruzuku ni mwaka mmoja, ukiwa na uwezekano wa kuongezwa kwa makubaliano kati ya wapokeaji wa ruzuku na Bodi ya Kili Challenge
- Ubunifu na utekelezaji unaotegemea ushahidi wa kisayansi
- Mashirika ya Kiraia (CSOs) yasiyoegemea upande wowote wa kisiasa
- Hatua za utekelezaji lazima zipangwe kwa kushirikiana na walengwa wenyewe
- Uwazi na uwajibikaji
- Ufanisi wa gharama: 85% ya ruzuku lazima ielekezwe moja kwa moja kwa miradi inayowanufaisha walengwa, huku 15% ikitumika kwa gharama za usimamizi wa ruzuku
- Uzingatiaji wa mazingira: Miradi itapitiwa ili kubaini athari hasi za kimazingira na kijamii, na ikiwa ipo, hatua za kupunguza athari hizo lazima zitekelezwe
- Msaada wa kiufundi wenye viwango vya juu na uwezeshaji wa jamii
- Miradi inayoongozwa na ushahidi wa kisayansi inapendekezwa zaidi
- Hatua za utekelezaji lazima zizingatie sheria na kanuni zote zinazotumika nchini Tanzania

**4. Vigezo vya Ustahiki**

- Mwombaji lazima awe Shirika la Kiraia (CSO) lililoundwa na WAVIU na linalofanya kazi katika Tanzania Bara.
- Waombaji wanaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima watambuliwe na halmashauri husika. Hivyo basi, kila ombi linapaswa kuambatana na barua ya utambulisho kutoka halmashauri husika.
- Mwombaji lazima awe na uthibitisho wa uadilifu wa hali ya juu na asiwe amehusishwa na vitendo vya rushwa au ufisadi, vinavyoadhibiwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Mwombaji lazima awe na mifumo thabiti na sahihi ya usimamizi wa fedha.
- Mwombaji lazima awe na muundo wazi wa utawala unaohakikisha uwajibikaji.
- Ombi lazima liandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**5. Kiasi cha Juu cha Ruzuku inayotolewa na mfuko wa Kili Challenge**

Ruzuku hii inapatikana kwa Mashirika hai ya Kiraia (CSOs), ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Kidini (FBOs), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Mashirika ya Kijamii (CBOs), na Mashirika ya Sekta Binafsi (PSOs) yaliyoanzishwa na Watu Wanaoishi na VVU (WAVIU) na kusajiliwa kisheria chini ya sheria za Tanzania. Mashirika yanayostahili kupokea ufadhili lazima yawe na anwani halisi na yawe yanapatikana ndani ya maeneo wanayokusudia kutoa hudumia ndani ya Tanzania Bara.

Kila kikundi au Konga ya WAVIU itakayotuma maombi ya ufadhili huu kinaweza kupokea kiwango cha juu cha **Shilingi 30,000,000 (Milioni Thelathini za Kitanzania)**. Vikundi au Konga ambazo zimeonyesha utendaji mzuri katika awamu za ufadhili uliopita zinahimizwa kuomba ili kuhakikisha mwendelezo wa utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI.

**6. Maombi ya Ruzuku**

Waombaji wanaostahili wanahimizwa kuwasilisha andiko la maombi yao kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kupitia Mamlaka zao za Serikali za Mitaa. Mamlaka ya Serikali za Mitaa inayosimamia eneo la utekelezaji wa mradi lazima itoe barua ya uthibitisho wa utambuzi wa waombaji, ambayo inapaswa kuambatanishwa na maombi.

Katika andiko la maombi, waombaji wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Jina la Shirika/Taasisi
- Anwani ya Mawasiliano, ikijumuisha jina la Wilaya na Mkoa
- Baruapepe
- Tovuti (kama ipo)
- Namba ya simu
- Jina na cheo cha mtu anayetuma maombi
- Tarehe ya kuanzishwa kwa shirika/taasisi
- Jina la Shirika la Ushirika (kama lipo)
- Historia ya ruzuku/ufadhili wa awali
- Eneo la huduma/Afua zinazotekelezwa
- Makundi lengwa, aina na idadi yao
- Idadi ya wafanyakazi wa kudumu na wa muda
- Je, taasisi inayoomba ina uzoefu wa kutekeleza miradi ya ruzuku au afua kama hizi?
- Lengo kuu na malengo mahususi ambayo mwombaji anataka kufanikisha ni yapi?
- Mbinu gani za jumla shirika/taasisi itatumia kubadili au kuboresha hali iliyopo?
- Ni kiwango gani cha rasilimali kinachoombwa kutoka kwenye ruzuku ili kuwezesha mabadiliko yanayotarajiwa (bajeti ya kina)?

**7. Uwasilishaji wa Tamko la Nia**

Waombaji waliopata barua ya uungwaji mkono kutoka kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) katika eneo ambalo mradi utatekelezwa wanapaswa kuwasilisha maombi yao yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwa TACAIDS.

Maombi yote yatatakiwa kuwasilishwa kwa njia ya mtandao na kuelekezwa kwa Mkurugenzi Mtendaji, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), S. L. P. 2904, Dodoma kupitia barua pepe barua@tacaids.go.tz. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni tarehe 22 Aprili, 2025, saa 5:59 usiku.